



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. No: DED/NMT/C/PCF 2/47/223

27/06/2022

TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo inapenda kutoa tahadhari kwa Wananchi wote kuwa hadi sasa haijatangaza Zabuni ya Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Staff Houses Tender)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo inapenda kuwafahamisha hivi sasa kuna taarifa inasambaa katika mitandao ikisomeka "Tender No PD/015/2021-2022/DED/W/04 CONSTRUCTION OF 24 STAFF HOUSES AT MBAWALA AREA IN THE NAMTUMBO DISTRICT" si rasmi, hivyo haitambuliwi na serikali

Aidha, zikiwepo Zabuni zitatangazwa kupitia tovuti ya Halmashauri www.namtumbodc.go.tz pia mitandao ya kijamii ya Halmashauri, redio, runinga na magazeti

Hivyo, Watanzania wote wenye nia ya kuomba zabuni za Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo wafuatilie mawasiliano rasmi ya Halmashauri pale zitakapotangazwa kupitia tovuti ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

Ikumbukwe kuwa, Zabuni zote zitafanyika bila Mwombaji kuombwa chochote na kupitia mfumo wa manunuzi ya serikali (TANePS)

Imetolewa na:


Chiriku H Chilumba
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
NAMTUMBO

